101 Hatua Katika Elimu Na Malezi

Othman Nuuri Topbash

Dar es Saalam - 2014

As-Salaam Islamic Center
Plot 354 Mbezi Beach, Makonde, Dar Es Salaam - Tanzania
Cell: +255 254 734 362,
Email: aic2013@gmail.com

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kutolesha sehemu yoyote ya toleo hili, kuitunza katika mfumo utakaowezesha kunakiliwa au kukisambaza katika aina au namna yoyote ile, iwe elektroniki, kuchapa, kunakilisha, kurekodi au vinginevyo bila kupata ruhusa kutoka kwa mwenye haki miliki.

ISBN: 978-9944-83-670-8

Mwandishi:	Othman Nuri Topbash
Msimamizi Mkuu:	Abdi Mohamed Adam
Mfasiri:	Ibrahimu H. Kabuga
Mhariri:	Saad Abdullah
Kupangiliwa vizuri na:	Sarkhan Isgandarov
	Nijat Garibov

101

Katika Elımu Na Malezı

Othman Nuri TOPBASH

Maneno Maridhawa kutoka ndani
ya Qur'an Tukufu yanasema:

"…Nawe fanya wema (kwa watu) kama Mwenyezi Mungu alivyo kufanyia wema wewe…"

(Al-Qasas, 28:77)

"Tena bila ya shaka mtaulizwa siku hiyo juu ya neema [uhai, mali, vipawa na suhula nyingine zote]."

(At-Takaathur, 102:8)

1

Malezi ya mtoto huanzia tumboni mwa mama. Hivyo, mlezi na mwalimu wa kwanza wa mwanadamu ni mama yake.

2

Watoto ni baraka kutoka kwa Mwenyezi Mungu ambazo wazazi na walimu wamekabidhiwa kama amana ili wawaandae kwa mwenendo mwema na maadili yaliyotukuka.

3

Maadili mema, tabia na shakhsia imara ndiyo urithi wenye thamani ya juu kabisa ambao wazazi wanaweza kuwaachia watoto wao. Njia ya kulifikia hili hupitia katika malezi ya kiwango bora na cha juu.

4

Katika viumbe wote, mwanadamu anahitajia zaidi malezi maalumu na maarifa. Kazi na sanaa bora kabisa katika maisha ya mwanadamu ni kulea na kutengeneza wanadamu wema na wazuri. Mwenyezi Mungu Mtukufu aliwatuma mitume Wake kama walimu, waelimishaji na walezi wakubwa kabisa wa mwanadamu. Kwa maneno mengine, kazi ya ulezi na ufundaji ni kazi ya mitume.

5

Mwalimu sio tu yule anayempa mwanafunzi taarifa juu ya mada fulani, bali ni yule pia anayepandikiza mbegu ya usafi, kufungua anga mpya, kujitambua, na kumfundisha tabia njema na maadili sahihi. Kwa maneno mengine, mwalimu ni yule anayejenga dhamiri salama na imara ndani ya mwanafunzi wake.

6

Katika kumlea mtoto, haitoshi tu kumpa mahali pa kulala na chakula kinachompa virutubisho. Hitajio kubwa zaidi kuliko yote ni kuupamba ulimwengu wake wa kiakili na kiroho kwa maarifa na mafunzo.

7

Mwalimu anatakiwa kumfundisha mwanafunzi wake kwa hali ya kiroho. Anatakiwa sio tu kumfanya mwanafunzi azipende taalumu za kidunia, bali pia mafunzo ya kidini, hali ya kiroho na hikma.

8

Elimu na mafunzo yanayotolewa kuegemea upande mmoja bila kuangalia upande wa kiroho ni yenye upungufu na kasoro. Kuna ulazima wa kuweka uwiano na mizania baina ya ulimwengu wa kimaada (wa kimwili) na ule wa kimaanawi (wa kiroho). Vinginevyo, kama ndege anayejaribu kuruka kwa kutumia ubawa mmoja, mwanafunzi naye atakuwa mawindo ya paka mwenye njaa.

9

Kila kiumbe anayeshindwa kwenda pamoja na mkondo wa maisha, lazima ataangamia na kupotea kabisa. Ndiyo maana Ali (r.a) alitupatia wosia ufuatao:

"Usiwalee watoto wako kuendana na mazingira ya zama zako, bali kuendana na zama watakazoishi."

10

Taifa linapokuwa na watu wachache waliofundwa vizuri na wenye kujitoa kwa moyo wote, taifa hilo litayapita mataifa mengine; la sivyo, litaendelea kubaki nyuma.

11

Haihitaji muujiza ili uweze kuuona mustakbali wa taifa. Inatosha tu kuwaangalia watoto na vijana wa taifa hilo. Kama wanatumia nishati na nguvu zao katika njia ya mambo mazuri, hali ya kiroho na wema, basi taifa hilo litakuwa na mustakbali wenye kung'aa. Kinyume chake, iwapo wanatumia nishati na nguvu yao kubwa katika kuyashibisha na kuyatosheleza matamanio yao ya kihayawani, basi mustakbali wa taifa hilo utakuwa wenye kusikitisha na wenye kuhuzunisha.

12

Wale wenye mtaji huwekeza katika eneo bora na lenye ufanisi. Hata hivyo, elimu ndilo eneo muhimu zaidi tunalotakiwa kuwekeza. Maandalizi sahihi kwa ajili ya mustakbali ni kuwatengeneza na kuwalea watu bora na wenye sifa adhimu.

13

Kitu cha kwanza ambacho mwalimu anatakiwa kuwa nacho ni shakhsia bora ambayo wanafunzi wataistaajabia na kuitamani; na anapaswa kueneza na kusambaza nuru, hali ya kiroho, maarifa na nishati chanya kutoka moyoni mwake, na awe na huruma na upendo wa hali ya juu kwa wanafunzi wake.

14

Mwalimu hawezi kuwa na taathira chanya kwa wanafunzi wake kama matendo yake yanapingana na maneno yake. Kama malenga maarufu wa Kituruki Ziya Pasha asemavyo:

“Kazi ya mtu ni kama kioo kinachoionesha tabia yake; hivyo usidanganywe na maneno tu.”

15

Mwelimishaji anapaswa kujipamba kwa mema anayowashauri wengine na ajitahidi kuwa mfano hai.

16

Lazima mlezi na mwalimu watengeneze nguvu chanya mahali walipo. Maisha ya baadhi ya wanyama ni mfano mzuri: kuku huwalinda na kuwahifadhi vifaranga wake chini ya mbawa zake wakati wa kuwalea. Nyoka huwatunza wanaye kwa macho yake. Nge huwabeba watoto wake mgongoni. Kama wanyama wanawaangalia watoto wao kwa umuhimu mkubwa kiasi hicho, vipi kuhusu wanadamu?

17

Hapawezi kuwa na elimu bora iwapo hakuna uaminifu baina ya mwalimu na mwanafunzi. Aidha, mwalimu anapaswa kuonesha shakhsia imara kwa watu wanaomzunguka kwa sababu watu huwapenda watu wa mfano na waliojipamba kwa shakhsia yenye kuvutia. Huwaadhimisha na kufuata nyayo zao.

18

Raia hutengenezwa kulingana na watu wanaowaongoza. Zama za Furaha (Asr Sa'adah) watu walitengenezwa kwa ruwaza za kiroho za Mtukufu Mtume (s.a.w). Maswahaba wa Suffa ni mfano bora wa jambo hili. Abdullah ibn Mas'ud, ambaye ni mmoja wa Maswahaba wa Suffa, alisema akionesha kiwango cha ukamilifu wa kimaanawi alichokifikia chini ya mafunzo ya Mtukufu Mtume (s.a.w):

"Tuliweza kusikia dhikr ya chakula wakati kikipita kooni."

19

Mikusanyiko ya kiroho kwa lengo la kutoa nasaha za kidini (suhba) ndiyo iliyokuwa njia kubwa ya Mtukufu Mtume (s.a.w) katika kuelimisha, kwa maana kulikuwa na mawasiliano ya kiroho katika mikusanyiko hiyo. Mikusanyiko hiyo ilikuwa ikitoa virutubisho vya kiroho vinavyohitajika kwa wale waliohudhuria. Hivyo, kutoa nasaha hizo ilikuwa sawa na kuwaandikia suluhu ya mahitaji yao.

20

Mwalimu anatakiwa kuuzingatia uwezekano wa kwamba mwanafunzi aliyekabidhiwa kama amana anaweza kuwa mtu mkubwa hapo baadaye; na asisahau kuwa huwenda anawafundisha watu mahiri wanaoweza kuleta mabadiliko ulimwengu.

21

Ili kutoa huduma yenye kiwango cha juu, mwalimu anatakiwa kuwa makini kuhusu kujiendeleza. Juhudi za kujiendeleza zinatakiwa tabia yake ya kawaida na endelevu. Vinginevyo, tunu na vipawa vingi vinaweza kudhoofika na kufifia kwa sababu ya uzembe wake.

22

Kizazi bora ni matunda ya walimu bora wanaoweza kutoa maarifa na maadili bora. Wale wanaofundishwa na walimu dhaifu na wasiokuwa na viwango watageuka kuwa watu dhaifu na wasiokuwa na sifa.

23

Tukitaka kutengeneza na kulea wanafunzi bora, tunatakiwa walimu bora.

24

Fundi hutambulika kwa kile alichokitengeneza. Vivyo hivyo, ubora wa mwalimu hutathminiwa kwa ubora wa mwanafunzi aliyemfunda.

25

Dhima kubwa kabisa ya mwalimu ni kujifunda vyema yeye mwenyewe, kwa maana mwalimu dhaifu hupoteza muda wa wanafunzi aliokabidhiwa.

26

Mchunga kondoo ana dhima kwa kondoo anaowachunga. Anatakiwa kumbeba kondoo aliyevunjika mguu. Vivyo hivyo, wanafunzi ni amana kwa walimu wao.

27

Kila mtu huamini kuwa maneno yake ni muhimu, yana thamani na yanatakiwa kusikilizwa na kuzingatiwa. Ndiyo maana mwalimu anatakiwa kuwa makini kumsikiliza mwanafunzi anayekuja kutaka msaada juu ya tatizo fulani.

28

Mwalimu anatakiwa kumchukulia mwanafunzi wake kwa uzito, amheshimu, na ajitahidi kwamba mwanafunzi wake alione hilo kupitia matendo yake.

29

Mwalimu anayemgeuza mwanafunzi wake kuwa kijiti kisichoweza kuwa mti mkubwa bila shaka atawajibika na atasailiwa mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

30

Mwalimu anapaswa kuzijua vyema tabia za wanafunzi wake kiasi cha kuweza kuutambua mshipa utakaompeleka kwenye nyoyo zao.

31

Kwa kuwa tabia na shakhsia zinatofautiana, mbinu au ushauri unaweza kumfaa mwanafunzi mmoja, lakini mbinu na ushauri huo huo unaweza kumdhuru mwengine. Ndiyo maana mwalimu anapaswa kuijua hali ya kiroho ya wanafunzi wake.

32

Mwalimu anapaswa kuvijua vipaji, vipawa na tunu za wanafunzi wake kama anavyovijua vipande vya tasbihi yake, ili aweze kuwaongoza kwenye uelekeo na njia ya vipawa vyao.

33

Leo tunaishi katika zama ambazo watu wanaelea kama vipande vya miti katika maji ya mafuriko bila kujua. La kusikitisha zaidi, mto unaoweza kuzipa uhai ardhi unazozipitia unatiririka kwenye mfereji wa maji machafu kwa sababu hayajaelekezwa kwenye uelekeo sahihi.

34

Mwalimu anapaswa kuwa mkarimu, mwadilifu na mwenye huruma kwa wanafunzi wake. Hatakiwi kuwapa mzigo mkubwa wa kazi wasioweza kuubeba. Anatakiwa kumuongoza kila mmoja kulingana na uwezo wake.

35

Mwalimu mwadilifu ni mwalimu wa darasa zima. Darasa haliwezi kuwa na amani bila uadilifu; darasa lisilokuwa na amani, hakuna somo linaloweza kufundishwa; mahali ambapo hakuna masomo yanayofundishwa, hapawezi kuwa na elimu.

36

Mwalimu anapaswa kujua vyema kwamba uadilifu sio kufanya usawa kwa kila mtu bali ni kumpa kile anachostahiki. Vilevile, mwalimu anatakiwa kujiepusha na tabia inayoweza kuvuruga na kuharibu hisia ya uadilifu.

37

Mwalimu anapaswa kuwa muadilifu, sio tu katika kutoa uamuzi, bali katika kutathmini mitihani. Kwa mukhtasari, anatakiwa kuwa muadilifu muda wote na katika mambo yote.

38

Mwalimu anatakiwa kuweka mipango kulingana na muundo wa darasa lake na nyenzo za masomo ili kwamba aweze kufundisha kwa ukamilifu.

39

Mwalimu mwenye mipango na nidhamu huweza kuona mahali alipoishia, kipi alichofundisha na ufundishaji wake umeleta matokeo ya aina gani.

40

Wakati wa kutengeneza mipango na programu mbalimbali, mwalimu anatakiwa kufikiria lini, wapi na namna atakavyoitekeleza mbinu zake ufundishaji.

41

Mwalimu anapaswa kujua kwamba dhima yake sio tu kuhamisha maarifa. Wakati wa kupangilia masomo yake, anapaswa kuandaa vipengele vitakavyowavutia wanafunzi. Kuwasilisha somo kwa kutoa mifano halisi na kutumia mbinu ya maswali na majibu itawafanya wanafunzi wawe wachangamfu na wasikivu.

42

Subira, ustahmilivu na kujitoa kwa moyo ni funguo muhimu kabisa za mafanikio katika elimu na malezi.

43

Mwalimu hapaswi kukata tamaa anapokabiliwa na tabu na ugumu; badala yake subira yake inatakiwa kuwa imara na madhubuti anapokutana na mazingira magumu.

44

Mwalimu hatakiwi kupoteza matumaini au kuonesha uzembe na unyonge Kwa sababu ya udhaifu na ukosefu wa nyenzo.

45

Ni lazima tusisahau kuwa siku zote maji ya uhai yanapatikana katika nyakati ngumu na maeneo ya shida na tabu; kwa maana kinachoyafanya maisha kuwa yenye thamani na ustawi ni juhudi na kujitolea katika njia ya kulifikia lengo tukufu.

46

Malezi sio upendo wa muda mfupi na wa kupita. Ni kazi tukufu kabisa inayotakiwa kutekelezwa kwa upendo na bidii mpaka pumzi ya mwisho. Katika kufanikisha hilo, subira inatakiwa kuwa ndio kirutubisho cha mlezi na Mwenyezi Mungu awe msaada wake.

47

Mwalimu ni mtu anayeweza kuilinda imani yake katika jamii yoyote ile anayoishi; anayeweza kuuepusha moyo wake usishughulishwe na mali na manufaa; anayeweza kuzisikia sauti za ukimya wa wale wanaopiga kelele ya kuhitajia elimu na malezi.

48

Kama ambavyo ni kosa kuwapuuza watoto, wazazi na kazi inayokupatia riziki kwa kisingizio cha kuwahudumia watu, vilevile ni kosa kutumia mambo hayo kama kisingizio cha kutowasaidia watu.

49

Mwalimu hatakiwi kuhuzunika kwa kukosa fursa za kimaada, wala kufurahia na kuharibiwa na wingi wa mali za kidunia.

50

Mwalimu anatakiwa kutenga muda kwa ajili ya wanafunzi wake nje ya muda wa masomo ya darasani. Asiwe kama mfanyakazi anayeingia na kutoka huku akisubiri zamu yake imalizike.

51

Mwalimu asiwe mtengenezaji wa matatizo bali awe mtatuzi wa matatizo. Badala ya kutafuta makosa na kasoro za kukosoa, anatakiwa kuyakabili mambo kwa moyo na mtazamo chanya.

52

Mwalimu asiwe mtu wa kuwalaumu wengine kwa makosa mbalimbali wakati wa kutoa elimu; anatakiwa kujiona kama chanzo cha makosa hayo.

53

Mwalimu kutafuta visingizio kwa kusema "nifanye nini? Sina uwezo wala vipawa. Ninapoteza muda. Hakuna anayekuja darasani kwangu," Mwenyezi Mungu huvijibu visingizio hivyo kwa kuumba mitini katika miamba na kutoa matunda kutokana na mitini hiyo.

54

Malezi ni sanaa ya kusahau visingizo mbele ya aina zote za shida. Malezi hayawezi kufanikiwa mahali ambapo ukosefu wa uvumilivu na visingizio hutawala.

55

Mwalimu mzuri hatakiwi kusubiri fursa suhula zimjie. Siku zote anatakiwa atafute nje za kuwahudumia watu.

56

Malezi na maadilisho sio kazi ya kukaa na kusubiri. Inahitaji kiwango cha juu cha nishati. Hivyo mwalimu anatakiwa kuujaza moyo wake kwa nishati chanya.

57

Mbegu za maarifa zinazopandwa kwa upendo na bidii hapo baadaye zitakuwa miti mikubwa ya mkuyu.

58

Mwalimu anatakiwa azijue vyema adabu na maadili yanayokubalika na kuheshimiwa na jamii na asizipuuze.

59

Mwalimu maridadi, mwenye adabu na moyo safi anatakiwa kuwahudumia watu kwa msisimko; asiziumize hisia za wengine na pia asiruhusu hisia zake ziumizwe kwa urahisi. Tukumbuke kuwa nyoyo ni mahali panapotazamwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu.

60

Mwalimu anatakiwa kuwa makini sana kwa kila tendo na mwanendo wake. Anatakiwa kuwa mtaratibu na mwenye adabu hata wakati wa kufanya mzaha.

61

Mwalimu mzuri anatakiwa kuijua mipaka myembamba iliyopo kati ya nidhamu na purukushani, staha na udhalili, heshima na ufakhari. Asivichangaye.

62

Katika kila hatua ya maisha, mwalimu anatakiwa afanye mambo kwa namna inayoendana na mwenendo wa Kiislamu. Asisahau kuwa kila anachofanya na kila analosema ni kama tofali linalowekwa katika shakhsia ya wanafunzi wake.

63

Mwalimu anatakiwa kujua kuwa elimu sio tu kuhamisha maarifa, bali pia kuhamisha tabia. Afikirie kuhusu makosa anayoweza kuambukiza wakati wa mchakato huu wa uhamishaji wa maarifa na muda wote ahisi kuwa atakuwa na dhima iwapo atahamisha na kuwaambukiza wanafunzi tabia na mwenendo mbaya.

64

Mwalimu anatakiwa kuwa mtu wa nyoyo anayefanya juhudi ya kutaka msamaha wa Mwenyezi Mungu kwa kuwasamehe wengine.

65

Kila mtu anahitaji upendo na huruma. Kuwahurumia na kuwapenda watu hupunguza uadui na kuongeza upendo na urafiki.

66

Malezi muafaka hayawezi kupatikana kwa mbinu za kifidhuli, zenye kuvunja moyo na ukali.

67

Ni jambo lisilokubalika kwa mwalimu kuwatesa wale walio chini yake kwa ajili ya kuwaadabisha.

68

Ukali uliopitiliza hutengeneza mfundo na kinyongo. Subira iliyopitiliza hudhoofisha mamlaka. Mafanikio hupatikana kwa kuweka uwiano mzuri baina ya mambo hayo mawili.

69

Mwalimu anapaswa kuzungumza kwa upole na uzuri, na daima azungumzie mambo mazuri. Kwa maana hakuna apendaye maneno makali na ya kifedhuli. Unyenyekevu, upole na maneno matamu ndiyo njia bora kabisa ya kuingia katika nyoyo za watu.

70

Kama ambavyo rubani asiyejisikia vizuri kisaikolojia hawezi kuruhusiwa kurusha ndege, mwalimu mwenye hasira au ambaye morali wake upo chini asiruhusiwe kuingia darasani.

71

Mwalimu anatakiwa kutoa maonyo na nasaha zake kwa amani na asisahau kuwa matendo na tabia zinazoumiza hisia za wengine ni ishara ya udhaifu mkubwa kabisa wa shakhsia yake.

72

Siku zote watu huathiriwa na hisia zao. Hufikiria na kufanya uamuzi kutokana na taathira hiyo. Hivyo, mwalimu mzuri anatakiwa afanye uamuzi baada ya kushauriana na wenzake. Hii inamuwezesha kutoa huduma sahihi..

73

Taathira ya mwalimu mwenye moyo uliojaa upendo na hali ya kiroho ni mfano wa taathira ya upepo mwanana unaovuma juu ya mabustani yaliyojaa maua yenye kunukia na kuyachukua manukato hayo mazuri mpaka sehemu za mbali.

74

Vitu vitatu huigeuza dunia kuwa Pepo: Huruma ya mikono yako, ulimi na moyo…

75

Katika kuufikia wokovu, waumini wenye ukomavu huwatafuta watu katika jamii na kuwapa elimu, kuwahudumia na kuwahurumia ili wapate kuokolewa.

76

Ushindi wa kweli ni ushindi wa nyoyo. Hili linaweza tu kufikiwa na wale wanaozigeuza nyoyo zao kuwa makazi ya upendo.

77

Mwalimu wa mfano ni mtaalamu wa nyoyo. Ni daktari anayezichanja nyoyo kwa chanjo ya uhai wa milele.

78

Moyo wa mwalimu unatakiwa kugeuka kuwa kitovu cha kiroho cha urekebishaji kwa kupata uwezo wa kuwatazama viumbe kupitia jicho la Muumba.

79

Upendo na juhudi hutatua matatizo yote. Tunawavuta watu ambao tumetatua matatizo yao. Tunapata thawabu kwa kila tunaemvuta na kubeba dhima kubwa ya yule tunayeshindwa kumvuta.

80

Kujitoa mhanga ni kipimo cha upendo.
Kuzungumza tu hakufai chochote.
Mawlana Jalaluddin Rumi anasema:
“Usiwe mpumbavu wa maneno.”
Madai ya kumpenda mtu yanatakiwa
kuthibitishwa kwa kujitoa.

81

Mwalimu anatakiwa kuhisi maumivu ya wanafunzi wake na kufurahi pale wanapokuwa na furaha. Awachukulie kama marafiki na ndugu. Pia anatakiwa kuijua lugha ya urafiki na udugu.

82

Mwalimu hatakiwi kuwa mtu anayetafuta makosa na kasoro za wanafunzi wake; bali awe mtu anayefanya juhudi za kuyarekebisha makosa yao kwa kutoyaweka hadharani.

83

Upendo ni kama mkondo unaoziunganisha nyoyo mbili. Utimamu wa elimu na malezo hutegemea nguvu za mkondo huu.

84

Mwalimu anatakiwa kuifungua sana milango ya moyo wake kwa ajili ya wanafunzi kiasi kwamba milango hiyo inaweza kutengeneza mkondo imara wa ushawishi na taathira kwao.

85

Upendo wa kuipenda elimu huongeza hamu katika kile anachokifundisha. Kuamiliana na wanafunzi kwa upendo na huruma humuwezesha mwalimu kufikisha ujumbe wake, sio kwa njia ya akili, bali kupitia njia za moyo.

86

Mwalimu anatakiwa kwenda darasani katika hali ya heshima kama anavyokwenda kwenye nyumba ya ibada. Atambue kuwa zana yake kuu ni upendo na udugu.

87

Elimu isiyofika moyoni haiwezi kugeuka kuwa maarifa na hekma.

88

Walimu hujenga mtazamo wa dunia katika viungo vya watoto vyenye thamani kubwa kabisa, navyo ni akili na moyo. Hivyo, ni sahihi kuwaita walimu kuwa "wajenzi wa mustakbali."

89

Maarifa na hekma vinaweza kuwa na taathira pindi unapoishi kwa moyo msafi na upendo. Unapofikia hali hii, huwaona wanafunzi wako kupitia miwani ya upendo na huruma. Mbegu zilizopandikizwa kwa upendo na huruma hudumu milele.

90

Ili uwe mwalimu mzuri, unapaswa kuwa na hisia madhubuti za upendo na huruma.

91

Wanafunzi wanatakiwa kutazamwa kama ndege waliovunjika mbawa na kuhudumiwa kwa upole na huruma. Kwa maana upole na huruma ni tiba mujarabu na madhubuti kabisa katika kulea akili na nyoyo salama na imara.

92

Huruma ni kama moto usiozimika ndani ya moyo wa mwalimu.

93

Ni dhulma kubwa kumteua kuwa mwalimu mtu mwenye ubinafsi na asiyekuwa na upole na huruma.

94

Kama ambavyo mandhari ya mawaridi na maua huzifanya nyuso za watu wakali kutabasamu, watu wanaowaongoza wenzao wanatakiwa kuwa na sifa za mawaridi na maua mazuri. Wawe na uwezo wa kuzilainisha nyoyo ngumu kabisa na kuzifanya nyuso zilizokunjamana zitabasamu.

95

Jambo muhimu kabisa ambalo mwalimu anatakiwa kulizingatia ni kujua kwamba makosa yanatokana na yeye mwenyewe na mafanikio hutoka kwa Mwenyezi Mungu.

96

Mwalimu anapaswa kuitazama kazi yake kama baraka na tunu kubwa kwake. Ili kuonesha shukran kwa kupewa baraka hii, anatakiwa kuwa na hisia ya kuwajibika kujiandaa kwa zana za kimaada na kiroho.

97

“Umimi” na “kujidai” vinatakiwa kuondoka na mahala pake mwalimu akawa na “upendo” na “upole”.

98

Maisha ya mwalimu yanatakiwa kujengeka kwenye msingi wa udhati, juhudi na kutoa huduma bila majivuno.

99

Kila siku ni ukurasa mpya na msafi kutoka katika kalenda ya maisha. Mikono yako ndiyo inayoujaza ukurasa huu kwa namna bora kabisa.

100

Mwalimu anatakiwa kuichukulia kila dakika anayokaa na wanafunzi wake kama pumzi yake ya mwisho katika ulimwengu huu na hivyo anatakiwa kuutumia muda huo namna iliyo nzuri. Awe na hisia ya kushukuru na aoneshe shukrani zake kwa vitendo.

101

Watoto wanahitaji malezi ya wazazi na walio wao katika ulimwengu huu, nao walimu na wazazi wanahitajia dua na sadaka zenye kuendelea (*sadaqatul – jaariyah)* za watoto hao huko Akhera.

Kutoka katika muongozo bora wa elimu na malezi

QUR'AN TUKUFU NA HADITH NA MJUMBE WA MWENYEZI MUNGU

Maneno bora ni Kitabu cha Mwenyezi Mungu.

Njia bora ni njia ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Uchamungu ndiyo ngao imara.

Mazungumzo bora ni kumdhukuru Mwenyezi Mungu.

Visa maridhawa ni visa vya Qur'an Tukufu.

Njea zenye nuru ni njia za Mitume.

Elimu bora na yenye manufaa ni ile inayogeuka kuwa maarifa na hekma.

Mali kidogo inayokufanya umshukuru Mwenyezi Mungu ni bora kuliko mali nyingi itakayokufanya umkufuru.

Kisingizo kibaya kabisa ni kile kinachotolewa wakati wa kufa.

Majuto mabaya kabisa ni yale ambayo mtu atakayokuwa nayo Siku ya Hukumu.

Uongo ni dhambi kubwa kabisa.

Utajiri bora ni utajiri wa moyo na kutajirika kwa kuridhika na kutosheka.

Imani bora ni ile iliyokita mizizi moyoni.

Mali bila kutoka sadaka na zaka itageuka kuwa fedheha siku ya Kiyama.

Kamari na riba ndiyo aina mbaya kabisa ya mapato.

Upofu mweusi kabisa ni kuipoteza njia baada ya kuingia kwenye njia ya haki.

Upofu mbaya kabisa ni upofu wa moyo.

Kumuongoza mtu kwenye njia iliyonyooka (Uislamu) ni bora kuliko chochote kinachochomozewa na jua. Haya ni matunda ya kuulea moyo.

Japokuwa aina zote za israfu zinazidiana kwa ubaya; aina mbaya kabisa ni "kumfayia israfu mwanadamu."